

## 10-Isti'aadhah Na Basmalah (Kuomba Kinga Na Kuanza Kwa Jina La Allaah):

إِسْتِعَاذَةُ وَالْبُسْمَلَةُ Isti'aadhah Na Basmalah (Kuomba Kinga Na Kuanza Kwa Jina La Allaah)

Ni vyema ieleteke kuwa inapasa kwa kila mwenye kutaka kuanza kusoma Qur-aan kuleta Isti'aadhah kusema:

أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَنِ الرَّجِيمِ

*A'uwdu bil-LLaahi minash-shaytwaanir-rajiym*

Najikinga kwa Allaah dhidi ya shaytwaan aliye baidishwa mbali na Rehma ya Allaah.

Iwe mwanzo wa Suwrah, au katikati ya Suwrah kutokana na amri ya Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿فَإِذَا قَرأتَ الْقُرْءَانَ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَنِ الرَّجِيمِ ﴾

((Unapotaka kusoma Qur-aan basi (anza kwa) omba kinga kwa Allaah dhidi ya shaytwaan aliyefukuzwa (kuwekwa mbali na Rehma ya Allaah kwa kusema: *A'uwdu biLLaahi minash-shaytwaanir-rajiym*))<sup>1</sup>)

Msomaji Qur-aan hutakiwa aisome Isti'aadhah *sirran* (kwa siri - kutotoa sauti); ikiwa anasoma kisomo chake bila ya kutoa sauti. Pia hutakiwa aisome kwa siri ikiwa anasoma hali ya kuwa yu peke yake iwe anasoma *jahran* (kwa sauti) au kwa siri (bila ya kutoa sauti). Ama ikiwa anasoma Qur-aan kwa kutoa sauti mbele ya hadhara ya watu wenye kumsikiliza atatakiwa aidhihirishe Isti'aadhah kwa kutoa sauti. Hali kadhaalika ikiwa kikundi cha watu wanaisoma Quraan mmoja baada ya mmoja kila mtu kusubiri zamu yake<sup>2</sup>, basi hutakikana msomaji wa kwanza kuisoma Isti'aadhah kwa kutoa sauti na waliobakia kuisoma *sirran* kila inapowadia zamu zao.

Wakati wo wote ule msomaji wa Qur-aan akitokezewa na jambo lolote lile la kupita lenye kumpelekea asite kusoma kisomo chake cha Qur-aan kama

---

<sup>1</sup> An-Nahl (16: 98)

<sup>2</sup>Ifahamike kwamba kukusanyika kusoma Qur-aan au du'aa kwa pamoja na sauti moja haipasi kabisa kwani hivyo ni uzushi. Hapo imekusudiwa ni kupeana zamu kila mtu anasoma kipekee akimaliza husoma mwengine mwenye zamu yake.

kwenda chafya, kukohoa, kupenga mafua au kueleza maneno yenye kuhusiana na kisomo chake mfano anapofasiri Qur-aan katika kikao cha darsa hicho hicho, huwa hatakiwi kuisoma tena Isti'aadhah.

Ama ikiwa jambo lililomtokezea ni katika mambo yasiyohusiana na Qur-aan, akashughulishwa mbali na Qur-aan, liwe la kuzungumza na mwenzake au kumjibu muulizaji, au kula au kunywa na kadhalika; basi ni vyema kuisoma tena Isti'aadhah atapotaka kuendelea na kisomo chake.

Asili ya utaratibu wa Isti'aadhah ni ile iliyokuja katika agizo la Allaah (سبحانه ) وَتَعَالَى<sup>3</sup> pale alipowaagiza wenyewe kutaka kusoma Qur-aan. Pia imethibiti nyongeza juu ya agizo la Allaah (سبحانه وَتَعَالَى) kutoka kwa Mtume (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ)<sup>4</sup>; hivyo inaruhusiwa kwa msomaji kuileta hiyo nyongeza kwa kuwa ni kamfuata Mtume (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ). Kwa hivyo, msomaji ana uhuru wa kuchaguwa kati ya matamshi haya:

أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَنِ الرَّجِيمِ

أَعُوذُ بِاللَّهِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

Kisha kufuatia Basmalah ambayo ni kutamka kamili::

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

BismiLlaahir-Rahmaanir-Rahiym.

Kwa Jina la Allaah Ar-Rahmaan (Mwingi wa Rehma), Ar-Rahiym (Mwenye Kurehemu)

---

<sup>3</sup>Aayah iliyo tangulia ya An-Nahl (16: 98)

4Kutoka kwa Abu Sa'iyd al-Khudri kwamba: "Alikuwa Mtume wa Allaah (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) anaposimama usiku akifunguwa Swalaah yake husema:

سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَحَمْدُكَ وَتَبَارَكَ اسْمُكَ وَتَعَالَى جَدُّكَ وَلَا إِلَهَ غَيْرُكَ

((Kutakasika ni Kwako, Ee Allaah, na Sifa njema ni Zako, na limetukuka Jina Lako, na Utukufu ni Wako, na hapana ilaah [mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki], asiyekuwa Wewe)), kisha huleta takbiyra ((الله أَكْبَر)) kisha husoma:

أَعُوذُ بِاللَّهِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

((Najikinga kwa Allaah As-Samiy'ul-'Aliym (Mwenye kusikia yote daima, Mjuzi wa yote daima) kutokana na shaytwaan aliyfukuzwa)) Imepokelewa na at-Tirmidhiy, katika mlango wa anayoyasema katika kufunguwa Swalaah, Hadith 242.